


# Hii ndio elimu?

Is this education?



© HakiElimu

**Waandishi/Authors:**

Lilian Kallaghe, Kathy Relleen and Godfrey Telli

**Mhariri/Editor:** Rakesh Rajani

**Kutafsiri/Translators:** Lilian Kallaghe and Godfrey Telli

**Mchoraji/Cartoonist:** David Chikoko

**Wachapishaji/Publishers:** HakiElimu

**Wasambazaji/Distributors:** HakiElimu and E&D Ltd.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yeyote ya kijitabu hiki kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala kwa HakiElimu.

Any part of this book may be reproduced for non-commercial purposes; provided attribution is made to the source and a copy of the publication is sent to HakiElimu.

**ISBN 998- 8943-5-6**



739 Mathuradas Road,

P.O. Box 79401,

Dar es Salaam, Tanzania.

Tel: (255 22) 2151852/3, Fax: (255 22) 2152449

Email: [info@hakielimu.org](mailto:info@hakielimu.org) Website: [www.hakielimu.org](http://www.hakielimu.org)

## **Shukrani za dhiti kwa wote waliotusaidia katika kutayarisha kijitabu hiki:**

- Ecoliers du Monde, Mwanza kwa msaada wao wa kuandaa majadiliano ya vikundi kuhusu "Shute nzuri ni ipi?"
- Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mchango wao wa mawazo kupitia barua pepe.
- Makampuni ya E&D Ltd na DTP Ltd kwa mchango wao wa mawazo kuhusu mpangilio.
- Wafanyakazi wa HakiElimu: Agnes Mangweha, Japhet Makongo, Emile Malinza, Frederick Rwehumbiza, Mariam Mwambalawa, Emmanuel Dedu na Ackland Zahabu.

## **Many thanks to all those who supported us in the production of this booklet:**

- Ecoliers du Monde, Mwanza for their support in holding focus group discussions on the subject of 'What is a Good School?'
- The NGOs and individuals that contributed their thoughts via e-mail
- E&D Ltd and DTP Ltd for their contribution on layout
- HakiElimu staff: Agnes Mangweha, Japhet Makongo, Emile Malinza, Frederick Rwehumbiza, Mariam Mwambalawa, Emmanuel Dedu and Ackland Zahabu



Kila mmoja anakubali kwamba elimu ni muhimu. Lakini ni elimu ya aina gani tunayohitaji? Elimu ni nini? Shule nzuri ni ipi? Mtoto anayepata elimu bora ana sifa gani?

Kijitabu hiki kina lengo la kuibua mjadala katika jamii kutokana na maswali haya. Ni moja ya mchango wetu kuimarisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM). Si lengo lake kuwakosoa walimu au viongozi wa elimu ila ni kutafuta njia zitakazosaidia kuboresha elimu. Katuni zimetumika makusudi ili kuwa kichocheo cha kufikiri zaidi.

Everyone agrees education is important. But what kind of education do we need? What is education? What is a good school? And what does an educated child look like?

This booklet aims to stimulate public discussion on these questions. It is one of our contributions to strengthen the country's Primary Education Development Plan (PEDP). It is not meant to criticise teachers or education officials but rather to explore ways in which we can improve education. The cartoons are deliberately stark to provoke thinking.



Kila mtoto Tanzania - bila kubaguliwa, awe masikini au tajiri, awe wa kijijini au wa mjini, mvulana au msichana, mwenye ulemavu au asiye nao - ana haki ya kusoma katika shule bora.

Hii ina maana kwamba hata mtoto mmoja asifukuzwe tena shule kwa sababu ya kushindwa kulipa karo au kwa sababu yoyote nyingine.


- **Kwa nini baadhi ya watoto wanashindwa kwenda shule?**
- **Wengine wanasema kwamba ni watoto wa matajiri tu ndio wana uwezo wa kujiunga na shule zilizo bora. Wewe unasemaje?**
- **Nini kifanyike ili kumwezesha kila mtoto kwenda shule?**
- **Ni jinsi gani tunaweza kuwapata watoto wengi zaidi wenye ulemavu kujiunga na shule?**

Every child in Tanzania - without discrimination, whether rich or poor, rural or urban, male or female, with or without disability - has a right to a good school.

This means no child should ever be turned away because of inability to pay or any other reason

- Why are some children unable to go to school?
- Some say that only rich children can afford to go to good schools. What do you think?
- What should be done to enable everyone to access schooling?
- How can we get more children with disabilities into schools?

# Hii ndio elimu?





Shule bora ni ile inayomjali mtoto, yenye mwamko wa kujifunza, ambapo kila mtoto anashiriki kikamilifu ndani na nje ya darasa.

- **Ni nini kinachochea mafunzo halisi shuleni?**
- **Wazazi na walimu wanaweza kufanya nini kuboresha mafunzo shuleni?**
- **Ni jinsi gani watoto wanaweza kuwa na sauti ya namna shule yao inavyoendeshwa?**

A good school is child-centered, with active learning, where children participate meaningfully inside and outside the classroom.

- What promotes real learning?
- What can parents and teachers do to support real learning in schools?
- How should children have a voice in the way their school is run?

# Hii ndio elimu?







Shule nzuri ni ile ambayo inamkaribisha na kumthamini kila mtoto, kumpa moyo wa kuwa wazi, kuuliza maswali, kufikiri, kuwa mdadisi na mbunifu. Shule ni mahali ambapo mtoto anapata elimu ya stadi za maisha na kuendeleza ubunifu.

- Ni nini kinachomfanya mtoto ajisikie anakaribishwa na kuhitajika shuleni?
- Kwa nini ni muhimu kwa watoto kuuliza maswali na kuwa na mtazamo wa kukosoa?

A good school is a place where every child is welcomed and celebrated, encouraged to be open, ask questions, think critically and be creative. It is a place which teaches life skills and fosters imagination.

- What makes a child feel welcome and wanted in school?
- Why is it important to have pupils ask questions and think critically?

# Hii ndio elimu?






Shule nzuri ni ile yenye walimu wanaojali, wenye uwezo na wanaojituma, wenye kutafakari na kuendelea kujifunza, wanaovutiwa na mazingira bora ya kazi na kuwajibika katika kazi zao. Ni sehemu ambayo uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi unadhihirishwa kwa kuaminiana na kuheshimiana.

- **Mwalimu bora ni yupi?**
- **Uhusiano kati ya walimu na wanafunzi katika shule zetu kwa sasa ukoje?**
- **Tutawasaidiaje walimu kufundisha vizuri zaidi?**
- **Walimu wanawezaje kuwajibika katika kazi zao?**

A good school has caring, competent and committed teachers, who are reflective and continually learning, who enjoy decent working conditions and ongoing support, and who are accountable for their work. It is a place where teacher-student relations are marked by trust and mutual respect.

- What makes a good teacher?
- What is the relationship like between teachers and students in our schools today?
- How can we help teachers to teach better?
- How can teachers be accountable for their work?

# Hii ndio elimu?





Shule nzuri ina miundombinu bora na vitendea kazi vya kutosha. Ina madarasa mazuri, vyoo, vitabu vya kutosha, vinavyoendana na mitaala na vinavyotia hamasa, maktaba na nafasi ya kutosha kwa burudani.

- **Kwa nini ni muhimu kusoma?**
- **Ni jinsi gani vitabu vinaweza kuandikwa ili kuwavutia zaidi wanafunzi?**
- **Muda na nafasi ya kucheza unamsaidiaje mwanafunzi kujifunza?**

A good school has decent infrastructure and adequate supplies. It has good classrooms, functioning toilets, sufficient, relevant and inspiring books, a library and plenty of opportunity for recreation.

- Why is reading important?
- How can school books be made more interesting for students?
- How does being given the time and space to play help a child to learn?

# Hii ndio elimu?





Shule nzuri ni mahali pa usalama na heshima kwa watoto wote. Ni sehemu ambayo watoto hawapigwi au kuadhibiwa kwa njia zinazowadhilisha. Ni sehemu ambapo watoto wote - hasa watoto wa kike na wenye ulemavu - hawabaguliwi, kuonewa na wala kunyanyaswa kijinsia na mtu yeyote yule.

- **Mwalimu, unajisikiaje unapompiga mtoto?**
- **Mwanafunzi, unajifunza nini unapopigwa?**
- **Je, walimu na wanafunzi wanawezaje kuheshimiana zaidi?**
- **Je, inawezekana kuwa na nidhamu bila viboko?**

A good school is a place of safety and dignity for all children. It is a place where children are not beaten or disciplined in other humiliating ways. It is a place where all children - especially girls and children with disabilities - do not face discrimination, bullying or sexual harassment from anyone.

- Teachers, how do you feel when you beat a child?
- Students, what do you learn from being beaten?
- How can teachers and students respect each other more?
- Is it possible to have discipline without beating?

# Hii ndio elimu?







Shule nzuri ni ile inayoongozwa vyema kwa njia za kidemokrasia, ni pale ambapo utawala ni shirikishi na unaihusisha jamii kikamilifu. Ni mahali ambapo watoto na wazazi wana sauti katika utawala wa shule. Ni sehemu ambapo rasilimali zinatumiwa vizuri kwa uwazi na uwajibikaji.

- Unashirikije katika uendeshaji wa shule yako?
- Je, unafahamu kamati ya shule yako inafanya nini na wajibu wake?
- Je, wazazi wanashirikije katika utawala wa shule?
- Je, unafahamu fedha za shule yako zinavyotumika?

A good school is well governed and democratic, where management is participatory and involves effective community engagement. It is a place where children and parents have a meaningful say in school governance. It is a place where resources are used well, transparent and accounted for.

- How are you involved in the running of your school?
- Do you know what your school committee does and is responsible for?
- How are parents involved in school governance?
- Do you know how your school funds are being used?

# Hii ndio elimu?






Shule nzuri ni muhimu kwa uraia bora - inahakikisha kwamba watoto wana ujuzi, ubunifu, msukumo na ari ya maendeleo yao wenyewe na maendeleo ya kidemokrasia kwa taifa zima.

- Je, elimu yetu inawaandaa wanafunzi kuwa raia hai wenye mwamko?
- Je, elimu inawezaje kutolewa kwa ubunifu zaidi?
- Je, elimu inawezaje kuwa ya kidemokrasia zaidi?

Good schools are crucial to vital citizenship - to ensuring young people have the skills, creativity, drive and aspirations that are essential to their own and the nation's democratic development.

- How can our education system teach students to be active citizens?
- How can children be educated creatively?
- How can education be made democratic?

# Hii ndio elimu?





Kila mmoja anakubali kwamba elimu ni muhimu. Lakini ni elimu ya namna gani tunayoitaka? Shule nzuri ni ipi? Maana ya elimu ni nini? Mtoto anayepata elimu bora ana sifa gani?

Haya ni baadhi ya maswali ya msingi katika kijitabu hiki. Ni ya muhimu si tu kwa viongozi wa elimu bali kwetu sisi sote.

Wewe unasemaje? Unajihusishaje na maswala haya? Jadilini kati yenu na kisha tuandikie. Tungependa kusikia kutoka kwako!

Kama tukiyatumia maoni yako katika machapisho yetu ya baadae tutakutumia zawadi ya fulana ya HakiElimu.

Usisahau kuandika jina kamili, jinsi, umri na anwani yako.

Everyone agrees education is important. But what kind of education do we want? What is a good school? What is the meaning of education? What does an educated child look like?

These have been some of the basic questions in this booklet. They are important not only for education officials, but all of us.

What do you think? What ideas do you have? Write to us, send us your thoughts; we want to hear from you!

If we use your ideas in any of our future materials we will send you a free HakiElimu T-shirt. Don't forget to include you name, address and age.

Andika kwa/Write to:

HakiElimu Machapisho/Publications

SLP/PO Box 79401

Dar es Salaam, Tanzania

Baruapepe/E-mail: [info@hakielimu.org](mailto:info@hakielimu.org)





**Kama shule yako  
inachusha..... ipambe!**

if your school is boring  
...give it some colour!



## **HakiElimu ni nini?**

HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika elimu kwa kuwezesha jamii kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera za elimu, kuimarisha ubunifu wa uendeshaji wa mijadala ya umma, kufanya utafiti yakunifu, wenye kuhoji, wenye kuchambua, kutetea na kushirikisha wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

## **What is HakiElimu?**

HakiElimu is a civil society organisation which works to realize equity, quality, human rights and democracy in education by facilitating communities to transform schools and influence policy making, stimulating imaginative public dialogue and organizing for change, conducting critical research, inquiry, analysis and advocacy, and collaborating with partners to advance common interests and social justice.



Distributed by:

